

Chanjo za COVID-19: Maswali Yanayoulizwa Sana kuhusu Dozi ya Pili ya Kiongeza Nguvu

Waraka huu unajumuisha maelezo na mapendekezo ya dozi ya kiongeza nguvu cha chanjo ya COVID-19 kwa wale wanaostahiki kupata [dozi ya pili ya kiongeza nguvu](#). Ikiwa bado [hujakamilisha](#) chanjo yako ya COVID-19 [awamu ya kwanza](#) na/au umepata [dozi yako ya kwanza ya kiongeza nguvu](#), basi hustahiki dozi ya pili ya kiongeza nguvu kwa sasa.

Je, dozi ya pili ya kiongeza nguvu ilianza kupatikana lini?

Tarehe 29 Machi, 2022, [Food and Drug Administration \(FDA\)](#) ya Marekani iliidhinisha dozi ya pili y kiongeza nguvu ya chanjo ya Pfizer-BioNTech au Moderna COVID-19 kwa watu walio na miaka 50 au zaidi na watu ambao kingamaradhi yao imeathiriwa (wale ambao mfumo wa kingamaradhi ni dhaifu). Kufuatia idhini ya FDA, [Centers for Disease Control and Prevention \(Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, CDC\)](#) vilisasisa mapendekezo yavyo ya COVID-19 ili kuruhusu watu fulani walioathiriwa kingamaradhi na watu walio na zaidi ya miaka 50 waliopata dozi ya kwanza ya kiongeza nguvu angalau miezi minne iliyopita ili kustahiki kiongeza nguvu kingine cha mRNA (au dozi ya pili ya kiongeza nguvu). Vilevile, CDC ilipanua mapendekezo yake ya dozi ya kiongeza nguvu cha mRNA ili pia kujumuisha watu wazima ambao walipata chanjo ya msingi na dozi ya kiongeza nguvu ya chanjo ya COVID-19 ya Johnson & Johnson angalau miezi minne iliyopita.

Je, ni nani anayestahiki dozi ya pili ya kiongeza nguvu?

Kwa sasa, kuna makundi matatu ya watu yanayostahiki kupokea dozi ya pili ya kiongeza nguvu ya chanjo ya COVID-19. Makundi haya ya watu ni pamoja na watu ambao huenda wakawa kwenye hatari ya juu ya ugonjwa mbaya, kulazwa hospitalini na kifo kutokana na maambukizi ya COVID-19. [Kulingana na FDA](#), ushahidi wa sasa unapendekeza onyo la kinga kwa muda mrefu dhidi ya matokeo mabaya kutokana na COVID-19 kwa wazee na watu ambao mfumo wao wa kingamaradhi umedhoofika. Watu wanahitaji kuzingatia umri na hali ya afya wakati wa kuchagua ikiwa watapata au hawatapata dozi ya ziada ya kiongeza nguvu. Wakazi wa North Dakota wanahimizwa kufanya mazungumzo na daktari wao au mtoa huduma wa afya anayeaminika ili kuhakikisha kuwa wanafanya uamuzi bora wao wenyewe.

1. Watu wote wazima walio na miaka 50 na zaidi

Watu wazima wote walio na miaka 50 na zaidi wanastahiki kupata dozi ya pili ya kiongeza nguvu ya chanjo ya COVID-19 ya mRNA (Pfizer au Moderna) [angalau miezi minne](#) baada ya dozi yao ya kwanza ya kiongeza nguvu ya chanjo yoyote ya COVID-19 iliyoidhinishwa.

2. Watu wote walio na miaka 12 na zaidi ambao mfumo wao wa kingamaradhi umedhoofika

Watu wote walio na miaka 12 au zaidi ambao [kingamaradhi ni ya wastani au imedhoofika vibaya](#) wanastahiki dozi ya pili ya kiongeza nguvu ya chanjo ya COVID-19 ya mRNA (Pfizer au Moderna) [angalau miezi minne](#) baada ya dozi yao ya kwanza ya kiongeza nguvu. Kwa sasa, vijana waliobalehe walio na miaka 12-17 wanaidhinishwa tu kupata chanjo ya Pfizer COVID-19 kwa dozi zote zinazojumuisha dozi zao za msingi, dozi ya ziada na dozi za kiongeza nguvu. Ikiwa kingamaradhi ni ya wastani au imedhoofika vibaya na hujapata [dozi yako ya ziada](#), lazima ufanye hivyo kabla ya kuomba dozi ya kiongeza nguvu. Tafadhali rejelea mtoa huduma wako wa afya ikiwa una maswali kuhusu ikiwa hali yako ya afya inakuruhusu kama mgonjwa ambaye kingamaradhi ni ya wastani au imedhoofika vibaya.

3. Watu wazima wote walio na miaka 18-49 ambao wamepata dozi mbili za chanjo ya COVID-19 ya Johnson & Johnson

Watu wazima wote walio na miaka 18-49 ambao walipata chanjo ya COVID-19 ya Johnson & Johnson kwa dozi yao ya msingi na dozi ya kwanza ya kiongeza nguvu [angalau miezi minne iliyopita](#) wanastahiki kupata dozi ya pili ya kiongeza nguvu ya chanjo ya COVID-19 ya mRNA (Pfizer au Moderna). Mwongozo huu HAUJUMUISHI watu wazima waliopata chanjo ya COVID-19 ya Johnson & Johnson kwa dozi ya yao ya kwanza lakini wakapata dozi ya kwanza ya kiongeza nguvu ya chanjo ya COVID-19 ya mRNA (Pfizer au Moderna).

Je, kwa nini nihitaji la pili la kiongeza bfuvu?

Kuna sababu kadhaa za kwa nini huenda ukataka kupata dozi ya pili ya kiongeza nguvu ikiwa unastahiki. Uamuzi wako utategemea kiwango chako binafsi cha hatari inayohusishwa na maambukizi ya COVID-19, ikiwemo ikiwa uko au huko kwenye hatari ya juu ya ugonjwa mbaya, kulazwa hospitalini na kifo na pia umri wako na wakati ulipata dozi ya mwisho ya chanjo ya COVID-19.

Kiongeza nguvu cha pili kinaweza kupunguza hatari yako ya kufa kutokana na COVID-19.

[Data kutoka Israeli](#) inabainisha kuwa dozi ya ziada (ya pili) ya kiongeza nguvu ni salama na inaokoa maisha. Vifo kutokanana kibadala cha omicron katika data hii vilikuwa vya kiwango cha chini sana—vilipungua kwa asilimia 78—kwa wale wa umri wa miaka 60 na zaidi nchini Israeli ambao walipata dozi ya pili ya kiongeza nguvu.

Hatari yako ya ugonjwa mbaya wa COVID-19 inaongezeka kutegemea na umri.

Kadri unapokuwa mzee, ndivyo dozi ya pili ya kiongeza nguvu inavyoweza kukufaa zaidi, kwa sababu kinga inayotolewa na chanjo za kiongeza nguvu hudidimia baada ya muda fulani. Katika kipindi chote cha janga, watu wazee wamekuwa na uwezekano zaidi wa kuugua sana kutokana na COVID-19. Watu wazee walio na COVID-19 wako kwenye ongezeko la hatari linalohitaji [kulazwa hospitalini](#), kulazwa chumba cha wagonjwa mahututi au vipumilio ili kuwasaidia kupumua. Vilevile, watu wazee wana [hatari kubwa zaidi ya 5x-340x ya kuaga dunia](#) kutokana na COVID-19, kutegemea na umri wao wakilinganishwa na watu wa umri wa miaka 18-29. Watu wazee na watu wanaoishi katika vituo vya utunzaji vya muda mrefu (kama vile makao ya maisha ya kusaidiwa na wauguzi walio na leseni) wanahimizwa kuzungumza na mtoa huduma wao wa afya kuhusu kupata dozi ya pili ya kiongeza nguvu.

Utendakazi wa chanjo baada ya kiongeza nguvu chako cha kwanza unaweza kuanza kudidimia baada ya muda fulani.

Utendakazi wa chanjo ya COVID-19 umeonekana kupungua baada ya muda fulani. Kwa hivyo, maafisa wa afya ya umma na wahudumu wa afya wanapendekeza umuhimu wa kuendelea kupata chanjo na kupata dozi za kiongeza nguvu wakati unastahiki. Wakati wa viwango vya juu vya wimbi la omicron, watu wazima [walikuwa na uwezekano wa chini wa asilimia 94](#) kuwekewa kipumilio au kuaga dunia kutokana na COVID-19 baada ya kupata chanjo tatu (au baada ya dozi yao ya kwanza ya kiongeza nguvu) wakilinganishwa na wale ambao walikuwa wamepata chanjo mbili pekee. Hata hivyo, kiwango hiki kilichotambuliwa cha kinga kinaweza kuanza kupungua baada ya muda fulani.

[Uchanganuzi wa CDC wa hivi majuzi](#) unaonyesha ushahidi wa kudidimia kwa kingamaradhi dhidi ya ziara kwenye chumba cha dharura na ziara za kulazwa hospitalini kutokana na COVID-19 wakati wa kipindi cha kuenea kwa omicron. Miezi miwili baada ya dozi ya tatu (au dozi ya kwanza ya kiongeza nguvu), watu walikuwa wamekingwa kwa asilimia 91 dhidi ya kulazwa hospitalini. Miezi minne baada ya dozi hiyo, kinga ilipungua hadi takribani asilimia 78. Kwa bahati nzuri, [utafiti](#) uliofanywa Israeli uliwapata waliopokea chanjo ya COVID-19 ya Pfizer au Moderna COVID-19 walikuwa na ongezeko la ~9-10-katika IgG na kingamwili za kusawazisha ndani ya wiki mbili za chanjo ya dozi ya pili ya kiongeza nguvu, kurejesha kingamwili hadi zile zilizopimwa baada ya dozi ya tatu ya chanjo. Hivyo, dozi ya ziada ya kiongeza nguvu inaweza kutoa kinga ya ziada.

Je, dozi za pili za kiongeza nguvu ni salama?

Data inaonyesha kwamba dozi ya pili ya kiongeza nguvu ya chanjo ya mRNA COVID-19 inaimarisha kinga dhidi ya COVID-19 mbaya na haihusishwi na masuala yoyote mapya ya usalama. FDA imetambua manufaa yanayojulikana na yanayowezekeka ya dozi ya pili ya kiongeza nguvu cha chanjo ya COVID-19 kwa chanjo yoyote kati ya hizi yanazidi hatari zinazojulikana na zinazowezekeka kwa makundi hayo ya watu.

Je, ninahitaji dozi ya pili ya kiongeza nguvu ikiwa nilikuwa na maambukizi ya COVID-19 awali?

Wakazi wa North Dakota wanahimizwa kuzungumza na mtoa huduma wao wa afya anayeaminika kuhusu ikiwa wanapaswa au hawapaswi kupata dozi ya pili ya kiongeza nguvu. Kutegemea na umri, hali yako ya afya, wakati ulipata maambukizi yako ya kwanza na kibadala cha COVID-19 ulichokuwa nacho, mtoa huduma wako wa afya anaweza kuamua ni vyema kuchelewesha dozi ya pili ya kiongeza nguvu.

CDC inapendekeza watu wapate chanjo hata ikiwa walipata COVID-19 awali. Wakazi wa North Dakota waliopatikana na COVID-19 baada ya tarehe 1 Januari, inawezekana waliambukizwa kibadala cha Omicron na wanaweza kuchagua kuchelewesha chanjo kwa miezi miwili hadi minne kabla ya kupata dozi ya pili ya kiongeza nguvu. Ushahidi unaojitikeza unapendekeza kinga bora dhidi ya ugonjwa wa COVID-19 ni kingamaradhi mseto, kuwa na chanjo na maambukizi ya awali. Ni vyema kuchanjwa kabla ya kuambukizwa ili kupunguza matokeo mabaya ya COVID-19.

Ni afya yako na ni uamuzi wako.

North Dakota Department of Health (Idara ya Afya ya North Dakota, NDDoH) inajitahidi kuupa umma rasilimali na nyenzo za elimu ili kila mtu afanye maamuzi ya kielimu na ufahamu kuhusu chanjo za COVID-19 na afya ya binafsi. Mapendekezo haya mapya ya dozi ya pili ya kiongeza nguvu yanawapa wanajamii wetu uhuru wa kuchagua ikiwa wangependa au wasingependa kupata dozi nyingine ya chanjo ya COVID-19 kutegemea na mambo yao binafsi ya hatari. Vipengee kama vile umri na maradhi yaliyopo vinaweza kuongeza uwezekano wa ugonjwa mbaya, kulazwa hospitalini na kifo cha mtu kutokana na maambukizi ya COVID-19. Kwa wanajamii wengi ndani ya jamii wanaosalia kwenye hatari ya juu ya COVID-19, kupata dozi ya pili ya kiongeza nguvu kunaweza kuanza kuwasaidia kuwa na ujasiri wanaohitaji ili kurudi kwenye maisha ya kawaida zaidi kwa tahadhari.

Je, ninaweza kupata chanjo yangu ya pili ya kiongeza nguvu lini?

Maelezo kuhusu watoa huduma na kliniki za chanjo ya COVID-19 karibu nawe yanaweza kupatikana kwenye ukurasa wa NDDoH [COVID Vaccine Locator](#). Pia unaweza kuwasiliana na NDDoH Hotline kwa nambari 1.866.207.2880 kwa usaidizi. Kama kikumbusho, unaweza kupokea chanjo nyingine za kawaida zinazopendekezwa (shingles, pneumococcal) wakati mmoja na chanjo ya COVID-19.

JE, NANI ANAWEZA KUPATA KIONGEZA NGUVU?

CHANJO YA PRIMARY
SERIES COVID-19

Pfizer-BioNTech

Anayepaswa kupata kiongeza nguvu:

Kila mtu aliyefikisha miaka 12 na zaidi

Anayepaswa kupata dozi ya pili ya kiongeza nguvu:

Watu wa wazima walio na miaka 50 na zaidi

Wakati wa kupata kiongeza nuvu zako:

Angalau miezi ili baada ya kukamilisha awamu chache awamu ya kwanza ya CD19k

Ikiwa unastahki kiongeza ngumu, angalau miezi 4 baada ya kiongeza nguvu chako cha kwanza.

Kiongeza nguvu unachoweza kupata:

- Watu wazima wa miaka 18 na zaidi wanapaswa kupata chanjo ya mRNA COVID-19 (Pfizer-BioNTech au Moderna) kwa kiongeza nguvu cha kwanza mara nyingi*
- Lazima kiongeza nguvu cha pili kiwe chanjo ya mRNA COVID-19
- Matineja wa miaka 12-17 wanaweza kupata tu kiongeza nguvu cha chanjo ya Pfizer-BioNTech COVID-19

CHANJO YA PRIMARY
SERIES COVID-19

Modern

Anayepaswa kupata kiongeza nguvu:

Watu wa wazima walio na miaka 18 na zaidi

Anayepaswa kupata dozi ya pili ya kiongeza nguvu:

Watu wa wazima walio na miaka 50 na zaidi

Wakati wa kupata kiongeza nuvu zako:

Angalau miezi ili baada ya kukamilisha awamu chache awamu ya kwanza ya COVID-19

Ikiwa unastahki kiongeza ngumu, angalau miezi 4 baada ya kiongeza nguvu chako cha kwanza.

Kiongeza nguvu unachoweza kupata:

Kwa kiongeza nguvu cha kwanza, kwenye chanjo ya mRNA COVID-19 (Pfizer-BioNTech au Moderna) ndiyo inayopendelewa mara nyingi*

Lazima kiongeza nguvu cha pili kiwe chanjo ya mRNA COVID-19

CHANJO YA PRIMARY
SERIES COVID-19

Johnson &

Anayepaswa kupata kiongeza nguvu:

Watu wa wazima walio na miaka 18 na zaidi

Anayepaswa kupata dozi ya pili ya kiongeza nguvu:

Yeyote aliyepata chanjo ya J&J/Janssen COVID-19 kwa dozi ya msingi na kiongeza nguvu chako

Watu wazima wa miaka 50 na zaidi waliopata chanjo ya J&J/Janssen COVID-19 mara ya kwanza, bila kujali aina ya kiongeza nguvu walichopotea

Wakati wa kupata kiongeza nuvu zako:

Angalau miezi 2 baada ya kupata chanjo ya J&J/Janssen COVID-19

Ikiwa unastahki kiongeza ngumu, angalau miezi 4 baada ya kiongeza nguvu chako cha kwanza

Kiongeza nguvu unachoweza kupata:

Kwa kiongeza nguvu cha kwanza, kwenye chanjo ya mRNA COVID-19 (Pfizer-BioNTech au Moderna) ndiyo inayopendelewa mara nyingi*

Lazima kiongeza nguvu cha pili kiwe chanjo ya mRNA COVID-19

*Ingawa chanjo za mRNA zinapendelewa kwa kiongeza nguvu cha kwanza, chanjo ya J&J/Janssen COVID-19 inaweza kutumika mara nyingi.

Chanzo: [Miongozo ya CDC kuhusu Kiongeza Nguvu](#)